



Zab. 15 - Ee Bwana utuonyeshe

Zab 15: 5, 7, 8, 9, 10; 12: 2b na 11

M: Jeannot Amani Mulume



6



1. Ee Mungu, unilinde, kwa maana nakukimbilia.
Namwambia Bwana: "Wewe ni Bwana wangu".
Bwana ndiwe urisi wangu na kikombe changu:
Ndiwe unaye nilindia mali yangu.
2. Namtukuza Bwana aliyenipa shauri,
Kweli moyo wangu wanifundisha hata usiku.
Namweka Bwana daima mbele ya macho yangu.
Sitatikisika kwa maana yupo kuumeni kwangu.
3. Kwa hiyo moyo wangu waona furaha,
Nayo roho yangu yatoa shangwe, hata mwili wangu utapumzika salama.
Kwani hutaiacha roho yangu kuzimuni,
Wala hutamkubali mwamini wako aingie shimoni.
4. Kwangu hakuna heri, ila katika Wewe !
Unanionyesha njia ya uzima,
Wingi wa furaha mbele ya uso wako
Anasa za milele kuumeni kwangu.